# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
**TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA**

**Mtaa wa Mwenge,**
**S.L.P. 588,**
**54201 Mbozi - Songwe.**
**Simu: (025) 2580226**
**Nukushi: (025) 2580213**
**Barua pepe: rbcsongwe@pccb.go.tz**
**Wavuti: http://www.pccb.go.tz**

## TAARIFA KWA UMMA

**SONGWE - APRILI 14, 2020**

**TAKUKURU SONGWE YAFUATILIA MIRADI YA SHILINGI 6,176,856,896.49 NA KUOKOA SHILINGI 297,961,092**

***Ndugu Wanahabari;***

Ofisi ya TAKUKURU Mkoa wa Songwe kwa kipindi cha Januari - Machi 2020 imefuatilia miradi ya maendeleo yenye jumla ya thamani ya Shilingi 6,008,647,814.49. Hii ikiwa ni moja ya majukumu yake ili kuhakikisha kuwa fedha za miradi zinazotolewa na serikali zinafanya kazi kwa malengo kusudiwa na kuleta matokeo chanya ili kuleta maendeleo na tija kwa wananchi wa Tanzania.

Miongoni mwa miradi hiyo ni pamoja na mradi wa miundombinu ya maji Iyula wenye gharama ya Shilingi 5,139,543,867.69 ambao ulikutwa kuwa na kasoro za udanganyifu wa bei za nondo kuwa juu sana kuliko bei ya soko kwa wakati huo. Katika ujenzi wa matanki ya maji ya Iyula A, Iyula B na Senjele bei ya nondo kwa kilogram moja mkandarasi aliweka kwenye makisio ya gharama ya ujenzi (BOQ) zisizokuwa na uhalisia wa bei za soko za kipindi husika. Bei ya nondo ya 10mm ilisomeka shs. 78,000/= wakati bei halisi ya nondo hiyo ya 10mm sokoni kwa wakati huo ilikuwa ni shs. 7,800/= kwa kilogram. Kuzidishwa huko kwa bei kulipelekea kuongeza gharama ya mradi huo na hivyo kuisababishia Serikali hasara ya jumla ya shs. 297,961,092/=.

Mkandarasi aliyefanya udanganyifu huo ni kampuni ya STC Construction Company ya Dar es Salaam. Udanganyifu huo wa Mkandarasi ulifanikiwa pia kutokana na uzembe wa aliyekuwa Mkandarasi wa Maji wa Halmashauri ya wilaya ya Mbozi kwa kipindi hicho pamoja na wataalam walioshiriki kufanya tathmini ya zabuni hiyo kwa makusudi kufumbia macho udanganyifu huo wa kampuni ya STC Construction Company. Watumishi hao ambao walipewa kazi ya kufanya tathmini walipaswa kuona kasoro hiyo na kushauri kitalaam ili bodi ya zabuni na uongozi wa halmashauri waweze kujua na kuchukua hatua mapema kuzuia hasara hiyo isijitokeze.

**Ndugu Wanahabari,**

Baada ya kupokea taarifa hii, Ofisi yetu ilianza mara moja kuchunguza tuhuma hizi. Wakati uchunguzi ukiwa unaendelea Ofisi yetu iliagiza mamlaka husika iliyompatia kazi Mkandarasi kufanya mapitio (Review) ya mkataba hususan makisio ya bei (BOQ).

Baada ya kukaa na kufanya mapitio hayo ambayo Ofisi yetu iliwaelekeza, kwa pamoja walikubaliana kuwa fedha hizo kiasi cha shilingi 297,961,092/= ambazo zilikuwa zimeongezeka kinyume na uhalisia mzabuni hatalipwa. Hii imesaidia kupunguza ghrama ya mradi wa maji wa Iyula kutoka jumla shilingi 5,139,543,867.69 na kuwa shilingi 4,841,582,775.70. Kwa hiyo mtaona juhudi za TAKUKURU Mkoa wa Songwe ndizo zimesaidia kuokoa fedha hizo.

Miradi mingine iliyotembelewa ni Ujenzi wa Ofisi ya Wakala wa Huduma za Misitu (TFS) pamoja na nyumba ya watumishi wenye thamani ya shilingi 705,126,168/-; Mradi wa vyumba vitatu vya madarasa katika shule ya Kakoma wenye thamani ya shilingi 40,000,000/= iliyopo wilaya ya Ileje; Mradi wa ukamilishaji vyumba vya madarasa katika shule ya sekondari Mwakatati wenye thamani ya shilingi 13,977,778.80 pamoja na ujenzi wa vyumba vitatu vya madarasa katika shule ya msingi Sogea wenye thamani ya shilingi 60,000,000/= iliyopo Halmashauri ya Mji wa Tunduma; Mradi wa ujenzi wa nyumba viwili pamoja na Ofisi nne za walimu wenye thamani ya shilingi 25,000,000/= katika Shule ya Sekondari Saza pamoja na Mradi wa ujenzi wa nyumba viwili pamoja na Ofisi moja ya walimu wenye thamani ya shilingi 25,000,000/= katika Shule ya Sekondari Maweni zilizopo wilaya ya Songwe; Ukamilisha wa ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa shule ya sekondari Nzoka wenye thamani ya shilingi 14,000,000 pamoja na Ujenzi wa ukarabaati wa zahanati wa kijiji cha Isanga shilingi 154,209,082.50 katika wilaya ya Momba. Katika miradi hii ipo ambayo tayari imekamilka na mingine ujenzi unaendelea lakini yote ujenzi wake upo katika hatua nzuri.

***Ndugu Wanahabari;***

Katika kipindi husika, Ofisi yetu pia iliendelea na majukumu yake mengine ambapo katika Uchunguzi na Mashitaka Ofisi yetu ilipokea jumla ya taarifa 54 za malalamiko ya vitendo vya rushwa. Kati ya malalamiko hayo, malalamiko 20 (37%) yalipokelewa toka kwa wananchi kwa kufika ofisini moja kwa moja kuleta kero zao; malalamiko 15 (27.8%) yalipokelewa kwa njia ya simu; malalamiko 12 (22.2%) yalipokelewa toka vyanzo vingine na malamiko 7 (12.9%) yalipokelewa kwa njia ya barua. Pia imeendelea kuendesha kesi 09 zinazoendelea kusikilizwa katika Mahakama za Wilaya na Mkoa wetu.

Katika uelimishaji Umma kuhusu rushwa na madhara yake Ofisi yetu kwa kipindi cha Januari -Machi 2020 imeweza kufanya semina kwa Walimu Walezi wa vilabu vya Wapinga Rushwa wa shule za sekondari zote za Mkoa wa Songwe, semina hii pia ilijumuisha Maafisa Elimu wa Sekondari ngazi ya Mkoa pamoja na wilaya.

Mbali na kundi la walezi wa Klabu za Wapinga rushwa pia tuliweza kuelimisha makundi mengine ya Wanafunzi, Vijana, Wanawake, Wanachama wa Vyama vya Siasa pamoja na Watumishi wa Mashirika ya Umma na Mamlaka nyingine za Serikali zilizo katika Mkoa wetu. Katika kipindi husika tumeweza kufanya Mikutano 14; Semina 08; Ufunguaji na Uimarishaji wa Vilabu vya Wapinga rushwa 42; Uandishi wa Makala/ Habari 10; Maonesho 03; Kuongea na Vyombo vya Habari 02 pamoja na Kurusha vipindi vya Redio 01.

Kwa upande wa Utafiti na Udhibiti na Ofisi yetu kwa kipindi cha Januari - Machi 2020 imefuatilia mali na fedha za Vyama vya Ushirika (AMCOS) ambazo walikopa lakini bado hawajarejesha kwenye benki mbalimbali pamoja na fedha wanazodaiwa na wananchi kama taarifa ilivyotolewa mnamo tarehe 15.02.2020. Pia tumefanya chambuzi za mfumo kwenye Vyama vya Msingi vya Ushirika AMCOS katika Ofisi zetu zote za TAKUKURU zilizopo Mkoa wa Songwe yaani ya TAKUKURU wilaya za Ileje, Momba, Songwe Kituo Maalum Tunduma pamoja na Ofisi ya Mkoa. Pia Uchambuzi wa Mfumo wa ukusanyaji mapato ya serikali pamoja na manunuzi ya umma katika Halmashauri ya Mji wa Tunduma.

***Ndugu Wanahabari;***

Ofisi yetu kwa kipindi cha Aprili - Juni 2020 tumejipanga kuendelea kufuatilia fedha za Vyama vya Ushirika (AMCOS) ambazo walikopa lakini bado hawajarejesha kwenye benki mbalimbali. Pia kuendelea kufuatilia mapato ya Halmashauri yaliyokusanywa na watumishi kwa njia ya PoS lakini hawajaziwasilisha benki wala kwenye mamlaka husika.

Pia kwa kipindi hiki tumejipanga kuelimisha wananchi kuhusu madhara ya rushwa katika uchaguzi kwa kuzingatia kuwa mwaka huu mwishoni kutakuwa na uchaguzi mkuu wa kuchagua Madiwani, Wabunge pamoja na Rais.

***Ndugu Wanahabari;***

Tunawashukuru sana kwa ushirikiano wenu mnaouonesha kwa Ofisi yetu hususani kwa kutuletea taarifa za vitendo vya rushwa pindi mnapovisikia. Nipende kutoa rai kwa viongozi wote wa Vyama vya Ushirika (AMCOS) kuhakikisha kuwa fedha zote wanazodaiwa na benki mbalimbali pamoja na wanazodaiwa na wananchi wahakikishe zinawafikia wahusika kabla Ofisi yetu haijawafikia wao.

Nitoe wito kwa watumishi wa Halmashauri wanaosimamia miradi ya maendeleo kuhakikisha kuwa wanasimamia miradi hiyo kwa uaminifu na uadidlilifu ili kuwaletea tija wananchi amabayo serikali imekusudia kwa wananchi wake.

Ninawakushukuru nyote kwa kufika na kunisikiliza, ninaamini mtaifikisha taarifa hii kwa wananchi pamoja na watumishi wa umma ili kila mmoja atambue wajibu wake katika mapambano haya kwa ustawi wa maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika Taifa letu.

***Damas Suta,***
***Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Songwe***